Jua litasogezwa karibu na viumbe Siku ya Kiyama mpaka liwe karibu nao umbali wa maili moja

Imepokelewa kutoka kwa Mikidadi bin Aswadi -radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake amesema: Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu -rehema na amani ziwe juu yake- akisema: "Jua litasogezwa karibu na viumbe Siku ya Kiyama mpaka liwe karibu nao umbali wa maili moja.", Sulaim bin 'Amir akasema: "Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, sijui (kiwango) alimaanisha nini kwa "maili"? Je, ni umbali katika ardhi au ni kile kijiti kinachotumiwa kupaka wanja wa manga kwenye jicho." (Mtume) Akasema: "Kisha, watu watakuwa ndani ya jasho yao kulingana na matendo yao. Miongoni mwao, kuna ambaye litakuwa hadi kwenye vifundo viwili vya miguu yake. Na miongoni mwao, kuna ambaye litakuwa hadi kwenye magoti yake mawili. Na miongoni mwao, kuna ambaye litakuwa hadi kwenye nyonga zake mbili. Na miongoni mwao, kuna ambaye jasho (lake) litammeza kabisa."

[Sahihi] [Imepokelewa Imamu Muslim]

Ameeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake ya kwamba Jua litasogezwa siku ya Kiyama karibu na viumbe, mpaka liwe vichwani mwao kwa kiasi cha maili moja. Amesema taabii (Mwanafunzi wa swahaba) Saidi bin Aamiri: Wallahi sijui ni maili mbili zipi alikusudia, je ni masafa ya ardhi, ama ni maili (wanja) ambao hutumika kupaka macho? Akasema: Watakuwa katika jasho kulingana na amali zao; yuko miongoni mwao ambaye jasho lake litatiririka mpaka chini ya kongo mbili zake za miguu, na yuko ambaye jasho lake litatiririka mpaka magotini, na yuko ambaye jasho litakuwa katika kitovu chake na kiunoni kwake, na yuko ambaye jasho litafika katika mdomo wake na litamzuia kuzungumza. Amesema: Na akaashiria rehema na amani ziwe juu yake kwa mkono wake katika kinywa chake.

http://sunnah.global/hadeeth/sw/show/4289